TANGAZO LA SERIKALI NA. 139 la tarehe 23/2/2023

SHERIA YA MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA, (SURA YA 370)

# HATI YA UHAMISHO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))*

UHAMISHO WA VIWANJA VILIVYOSAJILIWA KWA JINA LA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA KWENDA OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA

Sura ya 370 na Sura ya 257

KWA KUWA, Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ikisomwa kwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, mali zote za Serikali zimewekwa chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina;

Sura ya 370

NA KWAKUWA, Rais anaweza, kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, kumpa Msajili wa Hazina maelekezo ya kuondosha mali za uwekezaji au mali yoyote inayomilikiwa na Msajili wa Hazina chini ya udhamini na Msajili wa Hazina akatekeleza maelekezo hayo;

NA KWAKUWA, Serikali imeona kuwa inafaa Kiwanja Na. 20 Kitalu K Sehemu II chenye Hati Na. 056019/56 (11382) na Kiwanja Na. 39 Kitalu K Sehemu ya II chenye Hati Na. 056019/31 (10753) vilivyopo Manispaa ya Moshi mkoa wa Kilimanjaro chini ya umiliki wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhamishiwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

HIVYO BASI, inaekezwa kama ifuatavyo:

*Tangazo La Serikali Na. 139 (Linaendelea)*

Jina

1. Hati hii itaitwa Hati ya Uhamisho wa Viwanja vilivyosajiliwa kwa Jina la Ofisi ya Msajili wa Hazina kwenda Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, 2024.

Uhamisho wa viwanja

2. Viwanja vilivyoainishwa katika Jedwali la Hati hii ambavyo kwa sasa vinamilikiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, bila uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, vinahamishiwa katika umiliki wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

*Tangazo La Serikali Na. 139 (Linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Mkoa | Hati Na. | Hati Miliki na Maelezo ya Kiwanja | Taasisi Inayohamishiwa |
|---|---|---|---|
| Kilimanjaro | 056019/56 (11382) | Kiwanja Na. 20 Kitalu K Sehemu II, Manispaa ya Moshi | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka |
| Kilimanjaro | 056019/31 (10753) | Kiwanja Na. 39 Kitalu K Sehemu II, Manispaa ya Moshi | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka |

KWA AMRI YA RAIS

Dodoma,
…………………., 2023

MOSES M. KUSILUKA
*Katibu Mkuu Kiongozi*